RIPOTI YA MKUTANO MKUU WA BUFFALO 2013

Hii ni ripoti ya Kiswahili. Maelezo zaidi itapatikana kwa wale wanaipenda ndani ya ripoti ya kifarasa ambayo kila anayependa ataomba kwenyi offisi ya uongozi.

Kwa ufupi, mkutano wa Buffalo uliyo fanyika tariki 6 na 7 mwezi wa saba mwaka huu (6 et 7 Jullet 2013), ulichukuwa hatuwa zinazo fwata hapa chini. Mazungumuzo ilianza kwa kuwakaribisha wageni watatu tulio waaalika kutuelezea kuhusu associations zao, na walipo maliza basi presidenti Samuel Shekanena akakaribisha wanamemba na akampa directeur Executif John Kapapi apane mpango wa mazungumuzo (ordre du jour). Hii mpango wa siku mbili ulisimamishwa na kukubaliwa na wote kama hivi: 1.) Rudilio ya hatuwa zilisho chukuliwa Dallas 2012; 2.) Ripoti ya mwaka mzima Juillet 2012 mpaka Juillet 2013; 3.) Badilisho ndani ya katiba kubwa na kubaliana na katiba ndogo ya ndini (Reglement d'ordre interieur); 4.) Usikilizano baada ya kuzaliwa vikundi mbambali ya makabila marekani; 5.) Kamati ya uchaguzi ku postes zote ndani za kamati, na 6.) Mahali pa mkutano wa 2014 na hatuwa (resolutions) za mwisho.

1. Kisha kupana shukrani kwa kazi ilio fanyika na wanamemba wa Buffalo na Rochester, presidenti Shekanena alimpa nafasi ndugu John Kapapi arudilie hatuwa zilizo chukuliwa Dallas. Baada ya kuzisoma, na madiliko machache, zilikubaliwa na kusimamishwa kama hivyo.
2. Ripoti ya mwaka huu ilinzishwa na presidenti Shekanena. Matatizo ilipatikana ndani ya kamati zote mbili, alisisitiza bwana shekanena. Lakini alishukuru walewote walio jitolea ki mali, ki mwili na kazalika ili jamii hili letu la Benebuvira liendee mbele. Halafu akampa bwana Kapapi nafasi aendelee. Ripoti ilionyesha kwamba:

- Juu ya familia 50 lifika ama gunduliwa ndani Marekani mwaka huu. Liste yawo imeongezea kwa liste tunayo ya watu wote.
- Ombi la statut 501 c (3) iliingizwa tariki 25 mwezi wa kumi na mbili ku IRS (department de revenues) na tunangojea majibu
- Siti yetu, www.benebuvira-usa.org ilianza kutumika tangia mwezi wa tano 2013. Watu wote waliombwa kusaidia mawazo ya kuindelesha vizuri waki ivisite na kutuo waonyo yawo kwenyi offisi ya kazi (conseil executif)
- Kufunguliwa kwa ndugu Muzaliwa Rushinga wa Michigan baada ya kumaliza mwezi karibu sita ndani ya jeli. Kamati zote zilishukuru Benebuvira kwa roho ya upendo kwa jamaa hili. Ndugu mwenyewe hakuwa ndani ya mkutano.

- Pia mchunga hazina mama na dada Elizabeth K. Ligogo alitowa ripoti ya pesa kama ifwatayo. Kwanza aliambia wanamemba kwamba michango ya mwaka ilikuwa kwa jumla 1480 $ USA kutoka kwa jamii hizi: Jean Paul Badiya Mugemuzi –IA (180$), Boumedien Kasha-IA (180$), John Kapapi –TX (170$), Toto Alimasi-TX (100$), Manyongo Selemani-MI (175$), Samuel Shekanena-MI (100$), Cesar Ligogo-MN (175$), Sila Ngulu –IL (170$), Mugoli Yvone Lenge-GA (75$), Ngulwe Alfani-MN (75$), John Rugabano-WA (80$). Kuongezea kwa pesa hizi manamemba wa jimbo la NY - Buffalo na Rochester- walitowa 981$ kutoka kwa jamii hizi: Steve bareka 80$, Kulwe 150$, Lebon Mgerwa 50$, Mabenga Senenda 175$, Kashindi Sadiki 50$, Gabriel Shalamba 100$, Gervais Mabenga 166$, Mwajuma Jumaini 100$, Bawili katembo 70$, na Mutambala Shekwa wa Mbinga 40$. Pesa hizi za jamii za NY zilitumikishwa kwa kuandaa mkutano wetu wa Buffalo 2013. Mtumizi ya peza hizi zote itatolewa kwa mkutano wa mwaka kesho.
- Pia mama Elizabeth alisimama tena kwa nihaba ya presidenti wa wamama Fatuma Alimasi na akatowa ripoti ya wamama walio jiandaa kujisaidia kama wamama wakati wa matatizo yanayo angaliwa wamama Benebuvira. Ripoti hii ilionyesha mchango mpaleo sasa wa 700$ USA. Pesa hizi zilitolewa na wamama wafwatawo: Fatuma Alimasi, Kita Tugabano (WA), Mugoli Yvone Lenge (GA), Busime Kitahaza (IA), Anifa Wedi (TX), Elizabeth N. K. Ligogo (MN), Marie A. Rukubiriza (TX), Furaha Sende (TX), Toyi Bawili (IL), Chantal Kanefu (TX), Fatuma Eca Bukiza (WA), Zawadi Ngulu (IL), Cecile Kasha (IA).

3. Kulikuwa badiliko kazaa ndani ya katiba ilio patikana wakani aliye tusaidia kutuma ombi la statut 501 aliongeza. Mabadiliko yenyewa machache tu yalikubaliwa. Kuhusu katiba ya ndani (reglements d'ordre interieur), bwana Kapapi ilisoma katiba yote na ikakubaliwa baada ya kukosowa mawazo fulanifulani. Katiba hii ya ndani iliombwa ipatikane kwa kifransa na Kiswahili na itatumwa kwnyi kila offisi ya jimbo zote tano. Hatuwa zingine ziko ndani ya hatuwa za mwisho
4. Kuhusu masikilizano. Ndugu Kasha na Selemani walisimama na kueleweza manamemba kwamba kumejitokeza vikundi wa kabila hapa kwetu marekani na itasababisha umoja wetu wa Benebuvira kutokuwa na nguvu pia kwenda kinyume cha lengo la kuunda Benebuvira yenyewe. Kasha kupana malalamiko na kueleza kwa kifupi namna sisi wote, wavira na Fuliru tuko wamoja, wanamemba walikaataa hakuna kundi linguine la kikabila litakalo kubaliwa hama marekani ila benebuvira tuu.
5. Mandate ya kamati zetu mbili inakwisha mwezi wa saba 2014. Uchaguzu mwingine utafanyika. Ndugu Manyongo Selemani alichaguliwa kusimamia kamati ya uchaguzi na watu wote wanaalikwa kuomba ama kujitokeza ili kusaidia jamii letu liiendee mbele kwa muda wa myaka mimgine mitatu.
6. Mkutano w mwaka kesho utafanyika **Michigan.** Ili simamishwa kwamba nafasi itakuwa ANN ARBOR, lakini ni wajibu wa wanamemba wa Michigan kuhasiliana na kutujulisha

nafasi ya mwishi kama kutakuwa mabadiliko yoyote. Kwa jumla , hatuwa (resolutions) hizi zilikamatiwa:

- **Hakuna kundi la kabila litaruhusiwa tena Marekani.** Wandugu wanaojikia wanamemba wa CECUVIRA hapa marekani ni wanamemba wa Benebuvira. Kwahiyo, kazi zote za Cecuvira zitakazo fanyika hapa marekani zinapashwa julikana kwa Benebuvira wote. Pia kazi yoyote za kuendelesha mila ya Kifuliru inapashwa vilevile pitia na kujuliswa kwa Benebuvira wite. Kwa hiyo, Presidenti Shekanena kwa nihaba yaw a Fuliru-Case culturelle Fuliru , na ndugu Wadesisi Fumbate na Gabriel Shalamba kwa nihaba ya wavira –Cecuvira, walitumwa kwenda kuwaambia kundi zao kutuma mtu mmoja (representant) atakaye simamiya mambo ya mila ndani ya kamati kuu ya Benebuvira Marekani. Mikutano yoyote ya CCFuliru ama Cecuvira inapashwa fahamishwa ku Benebuvira kupitia kamati zao. Ndugu hawa watatuma ripoti na majibu kutoka kundi mbili zihi ku kamati kubwa ama ku kamati ya kazi haraka sana.
- **Wamama** wataendelea kukutanana kama kawaida na kuongeya ili waenedeleshe lengo lawa ikiwa pia watajulisha kamati kubwa kazi wanazo itajia kufanya
- **Kuhusu matatizo ya kazi ndani ya kamati**, postes za vice-president na secretaire wa kamati ya kazi, zilizo simamiwa na ndugu JP Bwenge Majagira na Honda Kahindo Wa Nandage, hazikubadilishwa ama watu wengine kuchukuwa nafasi yayo. Ila wanamemba waliwashukuru kwa upendo wao, na waliwatuma ndugu Gervais Mbinga na Mutambala D. wa Mbiga (NY-Buffalo) na dada Louise Fulano (Syracuse-NY) kuwafikia ndugu Honda na Bwenge ili wawaulize shida yawo na kuwafahamisha kwamda kjamii bado linawahitaji. Ripoti itatolewa ku kamati kubwa
- **Wa Representants wa majimbo**, waliombwa kufanya juhudi ili malalamiko ya wanamemba ndani ya majimbo ipunguzwe. Wanamemba walitowa malalamiko kwamba wanao wasimamiya hawajulikane ama hawa jail kufahamu wa Benebuvira wanao ishi ndani ya mitaa yawo. Pia, wanamemba ndani ya majimbo wanamamlaka ya kusuma malalamiko yako ku kumati kuu kama hakuna hatuwa ingine itachukuliwa.
- **Ki Feza,** mchunga hazina ameombwa kufanya bidi ili afatiliye deni na michango ya mwaka Marekani. Wasimamizi wa majimbo wameombwa kusaidiana ili wanamemba waendelea kueleweshwa kuhusu faida ya kuwa na mfuko wa kufanya kazi na kusaidiana hapa Marekani. Kamati hii ya kuchunga hazina iliombwa ilipe deni ya 700$ ya ndugu Ernesto Akili iliyobaki wakati pesa za kumtolesha mdugu Muzaliwa haikuweza kuenea. Mchunga hazina dada Elizabeth alikubali kwamba 600$ iko tayari na alipewa ruhusa achuwe 100$ ili amalize deni hiyo. Akili aliyekuwa hapo alipewa shukrani kwa upendo wake.
- **Kamati ya kazi (comite executive)** iliombwa kuangaliya namna ya kuwakumbuka walio kufa ama kuuwawa ndani ya jimbo la Mashariki tangiya vita ya 1996 hata Sange.

- **Postes mbili za mila (representations culturelles)** zimefunguliwa ndani ya kamati kubwa ya Benebuvira ili kuangalia mambo ya mila- Cecuvira et Case culturelle Fuliru. Mambo yote kuhusu mila na kijamii yatafanyika chini ya mamlaka ya benebuvira hapa Marekani. Shekanena na Wadesisi na Gabriel wafanye nguvu wapeleke habari hizi kwa kundi zao na kutuletea watu wawili kuchukuwa taji hili
- **Tipoti na kartasi zote (documents za benebuvira)** zitapatika kwa luga ya kifaransa, Kiswahili na Kingereza. Mikutano yoye ya Benebuvira itafanyika kwa Kiswahili lakini wanamemba wanaruhusiwa kuongeya kwa ki Vira ama ki Fuliru .
- **Kuhusu katiba ndogo (R.O.I),** wanamemba walio huzuriya mkutano huu walikubaliana wote (100%) kwamba

a. Benebuvira yoyote akifishwa ama akifa hapa marekani, jamii la Benebuvira itachukuwa jukumu ya kumaliza kilio. Na kila Benebuvira anaeishi hapa Marekani atotowa mchango unaombwa. Habari zitatolewa kuanzia mtaa kilio kimepatikana, kasha msimamizi wa jimbo atajulishwa kasha atajulisha presidenti wa benebuvira kasha wa Benebuvira wote watajulishwa
b. Ikiwa Benebuvira aliyekufa ama aliye mpoteza mwnamemba hapa Marekani, alikuwa mwanamemba kamili (member effectif) kutowa michango ama kuhuzuria mikutano (mkutano mkuu ama reunions locales) ata ongezewa ingine 500$ ili kusaidia tatizi zingine. Lakini Kama mwanamemba huyu alikuwa member tuu (member de droit), hatapewa 500$
c. Ikiwa Benebuvira amefishwa inje ya Marekani, michango na habari zitaenda kama kawaida kufwatana na mila yetu, “wani wani”. Hakuna mtu atashurtishwa kutowa mchango bali kufwatana na kadiri ya horo na mfuko wake.
d. Kama Benebuvira alikuwa hajulikani lakini aliishi hapa Marekani, ama alikataa kujijulisha ndani ya jamii kubwa ya Benebuvira, na sasa akipata msiba, atasaidiwa kama inavyo kuwa desturi ya mila “wani wani”. Lakini jimbo lake likiamuwa kuchukuwa hatuwa ingine ile, haita kuwa jukumu ya jamii lote ya Benebuvira.
e. Iliombwa pia kwa kila Benebuvira anaeishi hapa Marekani aheshimie sheria ya inchi hii. Ikijulikana kama mwanamemba alijuwa sheria lakini sasa amefungwa sababu ya tabia yake, jamii la Benebuvira haita ingiliya jukumu ya kusaidia kumulipia atoke jela. Itakuwa jukumu ya kibinasfi ama marafiki ama jimbo lake, sababu benebuvira inapenda tuwa wa raia wazuri wenyi kufwata sheria

- **Mkutano mkuu wa 2014 ilichaguliwa kufanyika pa Michigan.** Tariki na saa zitajuliswa siku zijazo

Walio huzuria mkutano huu ni wafwatawo

1. Samuel Shekanena, Grand Rapids, MI
2. Colon Mushi, Fort Worth, TX

3. Mabenga Z & Matumaini Senenda + 10, Buffalo NY
4. Akili Ernesto, Grand Rapids MI
5. Manyongo Selemani, Ann Arbor, MI
6. Cesar & Elizabeth K. Ligogo + 4, Saint Paul, MI
7. John Kapapi, Cross Roads, TX
8. JP Badiya Mugemuzi, Cedar rapids IA
9. Lea Nathalie Ngunge, Cedar rapids IA
10. Gervais & Claudina Shegayo Mbinga + 11, Buffalo NY
11. Boumedien & Cecile Kasha + %, Cedar rapids, IA
12. Wadesisi Fumabate + 3, Cleveland OH
13. Lebon & Mme Mkerwa, Buffalo NY
14. Amisi Kashindi , Rochester, NY
15. George Namweru, Iowa City, IA
16. Kyuma B. M Mbeja, Temple, TX
17. Bawili Katembo, Buffalo NY
18. Steve Bareka & Josephine Kilozo, Buffalo NY
19. Dieudonne M. & Regina Wa S. Mbinga +4, Buffalo NY
20. Kiza & Josephine jebereza, Buffalo NY
21. Alain Mugushu Balegereza, Syracuse NY
22. Elizabeth Kasimu, Buffalo NY
23. Merveille Shegayo, Buffalo NY
24. Esther Kyevu, Buffalo NY
25. Joyi Kasha, Cedar Rapids, IA
26. Louise Fulani, Syracuse NY
27. Chance Katemo, Syracuse NY
28. Erick Mbirizi, Syracuse NY
29. Hussein Alimasi, Buffalo NY
30. Mwajuma Mumaini, Buffalo NY
31. Emmanuel Rukeba, Buffalo NY
32. Asiya Mambo, Buffalo NY
33. Kashindi Vote Sadiki, Buffalo NY
34. Toni Kashunga, Beaumont TX
35. Kulwe, Buffalo NY
36. Busime Kitahaza + 1, Cedar Rapids IA